# YALIYOMO

YALIYOMO 1
Ushairi 3
Sifa za ushairi 3
Umuhimu wa ushairi 3
Istilahi za ushairi 3
KATEGORIA ZA MASHAIRI 6
Mashairi ya jadi. 6
Mashairi huru/za kisasa 7
Ulinganishaji wa Shairi la Arudhi na Shairi Huru 8
BAHARI ZA MASHAIRI 8
Kulingana na idadi ya mishororo katika ubeti 8
Kulingana na idadi ya vipande katika mshororo 9
Kulingana na vina 10
Kulingana na mpangilio wa maneno 11
Kulingana na mizani 12
Bahari nyinginezo za ushairi 13
UCHAMBUZI WA MASHAIRI 14
Namna ya kuchambua mashairi 14
Masuala mengine muhimu katika uchambuzi wa mashairi 16
Lugha ya nathari/Lugha tutumbi/mjalizo 17
UHURU WA KISHAIRI 18
Maswali na majibu ya baadhi ya mashairi 19
USHAIRI WA 1 19
USHAIRI WA 2 20
USHAIRI WA 3 21
USHAIRI WA 4 23
USHAIRI WA 5 25
USHAIRI WA 6 26
USHAIRI WA 7 27
USHAIRI WA 8 28
USHAIRI WA 9 29

USHAIRI WA 10 31
USHAIRI WA 11 32
USHAIRI WA 12 34
USHAIRI WA 13 36
USHAIRI WA 14 38
USHAIRI WA 15 38
USHAIRI WA 16 40
USHAIRI WA 17 41
USHAIRI: WA 18 43
USHAIRI WA 19 45
USHAIRI WA 20 48
USHAIRI WA 21 50

## Ushairi

- Ushairi ni utungo wa kisanaa unaotumia lugha teule na mpangilio fulani wa maneno badala ya kutumia lugha natharia(mflulizo).
- Ni sanaa inayotambulishwa na mpangilio maalum wa vifungu ambao una mdundo maalum na aghalabu hutumia lugha ya mkato.
- Shairi ni utungo wa kisanaa ambao hutumia lugha teule na kushirikisha mpangilio maalum wa maneno ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Ni tungo za kishairi zenye maudhui maalum yanayomhusu mwanadamu na tabia zake.

### Sifa za ushairi

Sifa ni upekee fulani unaojitokeza katika kazi yoyote ile. Ushairi huwa na upekee wa aina yake ukilinganishwa na kazi nyinginezo za fasihi. Hivyo basi utanzu wa ushairi huwa na sifa kuu zifuatazo:

1. Hutumia lugha teule na ya mkato.
2. Hutumia tamathali tofauti tofauti za usemi.
3. Sio lazima ufuate kaida za kisarufi.
4. Lugha iliyotumiwa huweza kuibua hisia, yaani hugusa moyo wa anayesoma.
5. Huwa na mpangilio maalum kuanzia kwa vina, mizani, mishororo na beti.
6. Huweza kukaririwa ama kuimbwa
7. Huelezea mambo yanayohusiana na imani za watu katika jamii.

### Umuhimu wa ushairi

Mashairi huwa na umuhimu anuwai katika jamii. Baadhi yazo ni pamoja na:

1. Kukuza usanii wa lugha.
2. Kuelimisha jamii kuhusiana na masuala fulani.
3. Kuburudisha wasomaji.
4. Kuhifadhi kumbukumbu za matukio muhimu katika jamii.
5. Kukuza utamaduni.
6. Kuhamasisha na kuzindua watu mfano kuhusu kazi.

## Istilahi za ushairi

### Mizani

Ni idadi ya silabi au sauti zinazotamkika katika kila mshororo wa ubeti. Mashairi mengi ya arudhi aghalabu huwa na mizani 16 ingawaje huwa siyo lazima.

### Vina

Ni silabi za mwisho wa kila kipande cha mshororo. Huainishwa kama vina vya ndani/kati ama vina vya nje/mwisho. Vina huweza kufanana ama kutofautiana. Iwapo shairi lina vipande ziadi ya viwili, vina huainishwa kutegemea vipande kwa mfano vina vya ukwapi, vina vya utao, vina vya mwandamizi na vina vya ukingo. Vina huwa ni **muhimu** kwa sababu zifuatazo:

a) Huleta mdundo, ridhimu na hata burudani kwa msomaji.
b) Hutambulisha na kupambanua utanzu wa ushairi kwani vina hutumika tu katika mashairi.

*Hebu tazama mfano unaofuata.*

Kurukia si kuzu**ri**, maneno musiruki**e**,
Mutakuja zusha sha**ri**, makonde muyabugi**e**,
Mukimbie kwa ghuru**ri**, kama kuku mukimbi**e**,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.
Wasemapo majaba**ri**, maneno musiruki**e**,
Hasa walio jeu**ri**, kamwe musikurubi**e**,
Ndondi zitawaazi**ri**, na kwa Mola mutubi**e**,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.
(Abedi K.A)

Katika mfano huo, vina vya ndani ni '**ri**' ilhali vina vya nje ni '**e**'

### Kipande (vipande)

Ni kijisehemu katika mshororo. Mshororo huweza kuwa na kipande kimoja, vipande viwili, vitatu au hata vinne.

a) **Ukwapi** – ni kipande cha kwanza katika mshororo.
b) **Utao** – ni kipande cha pili katika mshororo.
c) **Mwandamizi** – ni kipande cha tatu katika mshororo.
d) **Ukingo** – ni kipande cha nne katika mshororo.

### Mshororo (mishororo)

Ni mstari au sentensi moja katika ubeti. Mistari hii inapowekwa pamoja hujumlisha ubeti. Ni kigezo hiki ambacho hutumika kuainisha aina za mashairi.

a) **Mwanzo** –ni mshororo wa kwanza katika ubeti. Pia huitwa **fatahi** ama **kifungua.**
b) **Mloto** – ni mshororo wa pili katika ubeti.
c) **Mleo** – ni mshororo wa tatu katika ubeti.

**Mshata (mishata)**

Ni mshororo katika ubeti wa shairi ambao haujakamilika haswa kimaana na hutegemea mwingine unaofuata ili kupasha ujumbe. Idadi ya mizani pia huweza kuwa si kamilifu ikilinganishwa na mishororo mingine.

**Sifa za mishata**

1) Huweza kuishia kwa alama za mdokezo.
2) Huwa fupi
3) Huwa na mizani michache ikilinganishwa na mishororo mingine
4) Haikamiliki kimaana yaani haitoi ujumbe kamili.
5) Humhitaji msomaji kuwaza jinsi ya kuukamilisha.
6) Humlazimu msomaji kusoma mshororo mwingine ili kupata ujumbe.

**Mistari kifu/toshelezi**

Ni mishororo inayojitosheleza kimaana bila kutegemea mishororo mingine. Vilevile idadi ya mizani huwa kamili katika mishororo yote.

**Kibwagizo/kiitikio/mkarara/kipokeo**

Aghalabu huwa ni mshororo wa mwisho katika ubeti ambao umerudiwarudiwa katika beti zote.

KWA NAKALA NZAMA YA USHAIRI NA MASWALI YAKE,TUMA UJUMBE AMA UPIGE SIMU 0724351706